

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



## WIZARA YA AFYA

### TAARIFA KWA UMMA

#### MWENENDO WA UGONJWA WA UVIKO-19 KWA KIPINDI CHA TAREHE 27 AGOSTI HADI 30 SEPTEMBER, 2022.

**Dodoma, 04 Oktoba, 2022.**

**Ndugu Wananchi**, Serikali kupitia Wizara ya Afya, imeendelea kuimarisha mapambano dhidi ya UVIKO-19 nchini na inaendelea kutoa taarifa kwa umma kuhusu mwenendo wa ugonjwa huu. Katika kipindi cha tarehe **26 Agosti hadi 30 Septemba 2022**, jumla ya visa vipya **478** vimethibitika kuwa na maambukizi ya UVIKO – 19 ikilinganishwa na visa **586** kwa kipindi cha mwezi mmoja uliopita kuanzia tarehe 30 Julai hadi 26 Agosti 2022, sawa na upungufu wa asilimia **18.4**. Aidha, katika kipindi hicho, hakukuwa na vifo ukilinganisha na kipindi cha tarehe 30 Julai - 26 Agosti 2022 ambapo kulikuwa na vifo **4** vilivyoriipotiwa kutokana na UVIKO-19.

**Ndugu Wananchi**, Mchanganuo wa takwimu katika kipindi cha tarehe 27 Agosti hadi Oktoba 1, 2022 unaonesha kuwa watu waliothibitika kuwa na ugonjwa huo walitoka katika Mikoa 17 ikiwemo; Dar es Salaam (**382**), Mwanza (**28**), Arusha (**23**), Mara (**8**), Dodoma (**5**), Manyara (**5**), Morogoro (**5**), Lindi (**4**), Mbeya (**4**), Singida (**3**), Pwani (**2**), Kigoma (**2**), Katavi (**2**), Ruvuma (**2**), Mtwara (**1**), Kilimanjaro (**1**) na Tanga (**1**). Aidha, jumla ya wagonjwa wanne (**4**) waliothibitika kuwa na UVIKO-19 walilazwa na wote walikuwa hawajapata chanjo ikiwa ni punguko la wagonjwa wanne ukilinganisha na wagonjwa **8** waliotolewa tarifa kwenye tamko liliopita.

**Ndugu Wananchi**, Serikali imeendelea kutoa huduma za chanjo ya UVIKO-19 nchini ili kuwawezesha wananchi kupata kinga dhidi ya ugonjwa huu. Kuanzia tarehe 27 Agosti hadi Oktoba, 2022 jumla ya **Watu 3,499,099** wenye umri kuanzia miaka 18 na kuendelea walipata dozi kamili ya chanjo ya UVIKO-19, hii ni pungufu ya asilimia 10.3 ukilinganisha na **Watu 3,902,839** waliopata dozi kamili katika wiki ya tarehe 30 Julai - 26 Agosti 2022. Wizara inaendelea kuwahimiza wananchi kupata na kukamilisha chanjo ya UVIKO-19 ili kuzuia kupata ugonjwa mkali hata kifo, pale mtu anapopata maambukizi.

**Ndugu Wananchi**, Wizara inatoa tahadhari kwa wananchi wote kuendelea kuchukua hatua za kujikinga na UVIKO – 19 ikiwa ni pamoja na:

- Kupata kwa wakati dozi kamili za chanjo ya UVIKO - 19
- Kuvaa barakoa pindi unapojisikia dalili za mafua ili kuzuia kusambaa kwa maambukizi.
- Kuzingatia usafi binafsi ikiwemo kunawa mikono mara kwa mara kwa maji tiririka na sabuni au kutumia vipukusi (sanitizer).
- Kuwahi kwenye vituo vya kutolea huduma za afya endapo utakuwa na dalili za ugonjwa huu
- Kuendelea kuchukua hatua za kujenga mwili kwa kufanya mazoezi na kula vyakula bora
- Kutoa taarifa za kuwepo watu wenye dalili za ugonjwa huu katika jamii kupitia namba ya simu ya bure **199**.

**Imetolewa na:**

  
Dkt. Aifello W. Sichaawe  
**MGANGA MKUU WA SERIKALI**